

LATRA, wadau kujadili nauli usafiri wa umma

Na MWANDISHI WETU

MAMLAKA ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa wito kwa wadau wa usafirishaji abiria, kuhudhuria mkutano wa kupokea maoni kuhusu mapitio ya nauli za usafiri wa umma kwa njia ya barabara.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mamlaka hiyo jana na kusainiwa na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, mkutano utafanyika kesho katika Ukumbi wa Karimjee jijini, Dar es Salaam.

LATRA ilisema mkutano huo ni muhimu kwa wadau wote wa usafirishaji kuhudhuria na kujadili mapitio ya nauli

baada ya kupanda bei ya mafuta hatua iliyoathiri utoaji huduma.

"Mkutano unatarajiwa kuanza saa 3:30 asubuhi katika Ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam. Pia, wadau watakaoshindwa kuhudhuria wataweza kushiriki kwa njia ya mtandao kupitia LATRA Online TV," ilisema.

Taarifa hiyo ilisema kutokana na umuhimu wa mkutano huo, wenye nia ya kutoa maoni au michango wayawasilishe kupitia barua pepe ya Mamlaka hiyo yafanyiwe kazi.

Taarifa hiyo ilisema hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko la bei ya mafuta ya petroli na dizeli kwa takribani

sh. 950 kwa lita, hatua inayoongeza gharama za uendeshaji kwa watoa huduma za usafiri hatua inayoathiri utoaji wa huduma.

Taarifa hiyo ilisema mkutano huo utatoa fursa kwa wadau kutoa maoni kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa, endapo gharama za mafuta zitaendelea kupanda ambayo yatasaidia LATRA kufanya uamuzi sahihi kuhusu mapitio ya nauli.

"Endapo mwenendo wa kupanda bei ya mafuta utaendelea, gharama za uendeshaji zitaongezeka zaidi, jambo litakalohitaji tathmini ya kina kuhakikisha nauli zinaendana na hali halisi ya

uendeshaji huku tukilinda maslahi ya watumia huduma na watoa huduma," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema mkutano huo utafanyika kwa kuzingatia Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, kinachoitaka Mamlaka hiyo kufanya mapitio ya tozo mbalimbali za huduma za usafiri ardhini, zikiwemo nauli za usafiri wa umma.

Aidha, ilisema kwa mujibu wa Kanuni za Tozo za LATRA za mwaka 2020 (GN Na. 82 7 Februari 7, 2020, watoa huduma wanaruhusiwa kuwasilisha mapendekezo ya mapitio ya nauli au Mamlaka yenyewe kuanzisha mchakato huo inapobidi.

NAULI MPYA?

LATRA, wamiliki mabasi wakutana

DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

Macho na masikio ya Watanzania sasa yameelekezwa kwenye kikao cha kesho kati ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) na wadau wa usafirishaji, kujadili hatima ya nauli za daladala na mabasi makubwa.

Wadau hao wanakutana kufuatia ongezeko kubwa la bei ya mafuta, ambalo wamiliki na wasafirishaji wanalalamikia kuongeza gharama za uendeshaji.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Dk Habib Suluo, amesema jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kuwa kikao hicho ni muhimu kwa pande zote kwa sababu kitatoa mwelekeo wa suala hilo linalogusa uchumi wa taifa. Amesema wanatarajia kukutana na wasafirishaji ili kusikiliza hoja zao, kisha kuzichambua kuona kama zina mashiko, kwa kuwa mamlaka ina utaratibu wa kudhibiti viwango vya nauli.

"Tunategemea kikao hicho kitakuwa kizuri kwa sababu kila upande utawasilisha hoja zake. Baada ya hapo mamlaka itaeleza kwa kina kama kuna sababu ya kuongeza nauli au la. Suala hili linagusa Watanzania wa kada zote.

"Kila mmoja ni shuhuda katika hili. Bei ya mafuta imepanda. Dar es Salaam imefika shilingi 3,820, mikoani hadi shilingi 4,000. Sisi sote ni watumiaji wa usafiri wa ardhini, ukiwamo mabasi ya mijini, daladala na yale ya mikoani pamoja na nchi jirani.

"Katika hali hii, mdhibiti ana jukumu la



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), Dk Habibu Suluo akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kikao cha kila mwaka na mamlaka hiyo mjini Kibaha mkoani Pwani mwishoni mwa wiki.

kutoa mwongozo na kuwataka wasafirishaji wawe watulivu. Tunafahamu vita vinavyoendelea kati ya Marekani, Israel na Iran ndiyo sababu kubwa ya kupanda kwa bei ya mafuta. Haijwahi kutokea katika historia ya nchi yetu bei kupanda kwa kiwango hiki. Bei ya mafuta hutolewa na EWURA," amesema.

Amesema kupanda kwa bei hiyo kunaweza kuathiri utoaji wa huduma mijini na vijijini, pamoja na usafirishaji wa mizigo, kwa kuwa magari ya biashara yanapaswa kufanya kazi kila siku.

"Mamlaka ilitarajia kupanda kwa bei hii, lakini kiwango kilichopanda ni kikubwa. Wapo walioanza kupandisha nauli bila

kuzingatia taratibu. Biashara inapobadilika ghafla, haimaanishi siku hiyo hiyo unaanza kupata hasara.

"Nawaomba wasafirishaji wawaone huruma Watanzania. Wapo wenye vipato vidogo, na hawa ndio wanachangia uwekezaji wao. Tusitumie hali hii kuwaumiza. Hata kwa imani zetu ni dhambi kutumia shida za watu kujipatia kipato.

"Katika kipindi hiki cha mpito, tunawasihi msipandishe nauli bila idhini ya mamlaka. Hatutasita kuchukua hatua kali kwa yeyote atakayekiuka sheria. Migogoro itatuliwe mezani. Hatujui hali itakuwaje mwezi ujao. Hili ni janga la dunia kwa sasa," amesema.

Ameleza kuwa Kanuni ya 9(2) ya

upangaji nauli inamtaka mtoa huduma kuwasilisha maombi kwa mamlaka endapo mrejesho wa mtaji wake utashuka chini ya asilimia 10 ndani ya kipindi kisichopungua miaka mitatu.

"Waje wathibitishie kwa hesabu zao kwamba kwa bei hii ya mafuta, mrejesho wa uwekezaji wao uko chini ya asilimia 10. Tunataka uthibitisho rasmi," amesema.

Amesema mamlaka itatoa nafasi kwa wadau wote kuwasilisha hoja zao na kusikiliza maoni ya watumiaji wa huduma hizo.

Ameongeza kuwa Kanuni ya 9(3) inaeleza kuwa iwapo mrejesho utashuka chini ya asilimia 10 kabla ya miaka mitatu kukamilika, mamlaka inaweza kuzingatia maombi hayo kwa uangalifu maalumu, huku akibainisha kuwa nauli za sasa zilitangazwa Desemba 8, 2023.

"Mtoa huduma aje na hesabu zake zilizo wazi. Aonyeshe mrejesho wa uwekezaji wake uko chini ya asilimia 10. Hivyo ndivyo utaratibu wa kupanga nauli unavyotaka.

"Mamlaka pia ina jukumu chini ya Kanuni ya 13(1) kupanga tozo hata kama maombi hayajawasilishwa. Tutatumia taarifa tulizonazo. Tutashirikiana na EWURA kufuatilia hali hii ambayo hatujui itaendelea kwa muda gani.

"Tusisahau wanaobeba mzigo huu ni Watanzania. Tunapaswa kuangalia uwezo wao wa kumudu gharama hizi, ikiwamo wanafunzi wanaotegemea usafiri kufika shule," amesema.

Amesisitiza kuwa waombaji wa marekebisho ya nauli wanapaswa kuwa na leseni hai, kuwasilisha viwango vipya vinavyopendekezwa, kueleza sababu za kuomba ongezeko, kuonyesha manufaa kwa watumiaji, pamoja na kuwasilisha hesabu zilizokaguliwa.

Katika hatua nyingine, Dk Suluo ameonya kuwa daladala au mabasi yatakayogoma kutoa huduma kwa kisingizio cha kupanda kwa bei ya mafuta au kupandisha nauli kinyume cha sheria, yatachukuliwa hatua kali, ikiwamo kufutiwa leseni.

BALANCING ACT Petrol now retails at Sh3,820 per litre, up from Sh2,864 in March—a 33.4 percent rise

Latra officials meet stakeholders to consider fare increase options

Latra faces a delicate task, balancing the sustainability of transport operations while ensuring that any fare increase does not trigger wider economic pressures

By Rosemary Mirondo
@mwaikama
rmirondo@tz.nationmedia.com

Dar es Salaam. With fuel prices reaching historic highs, the Land Transport Regulatory Authority (Latra) is set to meet transport stakeholders tomorrow, April 8, 2026, to discuss fare adjustments and the challenges facing the sector. Analysts note that the regulator faces a delicate task: balancing the sustainability of transport operations while ensuring that any fare increase does not trigger wider economic pressures that could affect other goods and services.

Petrol now retails at Sh3,820 per litre, up from Sh2,864 in March—a 33.4 percent rise. Diesel has increased to Sh3,806 from Sh2,858, while kerosene now costs Sh3,684, up from Sh2,932.

The sharp rise follows the February 28, 2026, US-Israel invasion of Iran, coupled with a blockade of the Strait of Hormuz by unfriendly nations. These events have disrupt-

ed global oil supply routes, pushing crude prices above \$100 per barrel, with Brent trading between \$105 and \$110. The increase has added pressure to the transport sector, which relies heavily on fuel for daily operations.

High fuel prices act like an indirect tax on consumers and businesses, reducing disposable income, slowing economic growth, and increasing inflation. Rising transportation costs in turn raise the price of goods and services, creating a ripple effect across the economy.

Transport operators, including bus owners, tricycle and motorcycle taxi operators, are expected to present proposals on fare adjustments at the Latra meeting. The discussions will also focus on operational cost pressures, service delivery challenges, and regulatory measures aimed at ensuring the sector remains functional despite soaring fuel prices.

The Secretary General of the

Tanzania Bus Owners Association (Taboa), Mr Priscus Joseph, said fare increases are inevitable but should remain modest and based on realistic cost calculations.

"Fares should be increased after careful calculation. Some operators have raised fares excessively, which could unduly burden passengers," he said. He also pointed out the lack of coordination among government institutions has worsened the situation, arguing that better preparation could have mitigated public frustration.

Mr Joseph highlighted that rising costs go beyond fuel, noting increases in battery prices, vehicle maintenance, and other operational expenses. "When you touch fuel, you affect everything," he said, stressing that fare adjustments must reflect true operational costs rather than speculative increases. He added that motorcycle taxi operators and tricycle (Bajaj) owners should also be reviewed, as some have raised fares disproportionately despite moderate fuel consumption.

Similarly, Tamstoa Secretary General Issa John urged the gov-

ernment to reduce taxes on fuel to ease the burden on traders and the general public. Dar es Salaam Regional Commuter Bus Owners Association Secretary, Shifaya Anselma, said the situation affects the entire country and emphasised the importance of dialogue. "It's not just about fuel prices. We need to sit down and discuss how to cope with these challenges. Dialogue can help reach a practical understanding," he said.

Tamstoa chairman Chuki Shaban echoed calls for short-term reductions in fuel-related levies, noting that such measures could help stabilise fares and reduce the impact on both operators and passengers. Meanwhile, Executive Director of the Tanzania Association of Oil Marketing Companies (Taomac), Raphael Mgaya, warned that citizens should prepare for further increases in fuel prices.

He said the current rates are supported by previously imported fuel still in circulation, and the next wave of imports will likely push prices higher. Mr Mgaya also suggested that institutions capable of allowing employees to work

remotely should consider doing so to reduce fuel demand and consumption. "Next month, all goods are likely to become more expensive as fuel prices continue to rise. This situation is unprecedented in Tanzania's oil sector and requires collective planning and adaptation," he said.

Latra's role

As Latra convenes tomorrow, the meeting will serve as a critical platform for stakeholders to weigh the immediate need for fare adjustments against the broader economic impact. Analysts emphasise that a coordinated approach is essential to protect consumers, support operators, and maintain stability in the transport sector.

The meeting is expected to bring together key government officials, bus and truck owners, operators of tricycles and motorcycle taxis, and other stakeholders, providing an opportunity to discuss both short-term measures and long-term strategies to mitigate the effects of rising fuel costs. Observers say the regulator must ensure any fare increases are measured, transparent, and justified by operational realities to avoid further inflationary pressures.

In the coming weeks, citizens and businesses will closely monitor the outcomes of the Latra meeting, which could set the tone for how Tanzania navigates one of the most challenging periods for its transport and logistics sector in recent years.

Habari Leo Jumanne Aprili 7, 2026 Pg 2

Latra kuanza kupokea maoni ya nauli kesho

Na Ikunda Erick

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kesho itanza mchakato wa kupokea maoni ya wadau kuhusu uwezekano wa kufanya mapitio ya nauli za usafiri wa umma, baada ya kupanda kwa bei ya mafuta na wadau kulalamika kunachangia kuongezeka kwa gharama za uendeshaji kwa watoa huduma.

Taarifa ya umma

iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Latra, Habibu Suluo jana Dar es Salaam ilisema bei ya mafuta ya petroli na dizeli imeongezeka kwa takribani Sh 950 kwa lita, hali inayotishia kuathiri utoaji wa huduma za usafiri ikiwa haitapatiwa ufumbuzi wa haraka.

Suluo alisema kuwa endapo mwenendo wa kupanda kwa bei ya mafuta utaendelea, ni wazi kuwa gharama za uendeshaji zitaongezeka zaidi na hivyo

kuathiri sekta nzima ya usafiri wa umma, jambo linaloweza kusababisha hitaji la kurekebisha nauli ili ziendane na hali halisi ya kiuchumi.

Alifafanua kuwa Latra kwa kuzingatia Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, ina wajibu wa kufanya mapitio ya tozo mbalimbali za huduma za usafiri, ikiwemo nauli, kwa kuzingatia maslahi ya watumiaji na watoa

huduma kwa wakati mmoja.

Kutokana na hali hiyo, mamlaka hiyo imeitisha mkutano wa wadau unaoanza kesho Aprili 8, mwaka huu katika Ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam, kuanzia saa 3:30 asubuhi.

Suluo alisema lengo ni kukusanya maoni yatakayosaidia kufanya maamuzi sahihi kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa.

"Maoni ya wadau ni muhimu katika kuhakikisha

kuwa nauli zitakazopendekezwa zinaakisi gharama halisi za uendeshaji huku zikilinda maslahi ya wanaochi," alisema Suluo.

Aidha, Latra imeeleza kuwa wadau watakaoshindwa kuhudhuria mkutano huo ana kwa ana watapata fursa ya kushiriki kwa njia ya mtandao kupitia Latra Online TV, huku wale watakaotaka kuwasilisha maoni yao wakihimizwa kuyatuma kupitia barua pepe rasmi za mamlaka

hiyo.

Kwa mujibu wa Kanuni za Tozo za Latra za mwaka 2020, mchakato wa mapitio ya nauli unaweza kuanzishwa na mtoa huduma au mamlaka yenyewe pale inapobidi, ili kuhakikisha huduma za usafiri zinaendelea kuwa endelevu bila kuwaumiza watumiaji.

Kupanda kwa bei ya mafuta kumetokana na athari ya vita vinavyoendelea Mashariki ya Kati.